
East African Journal of Swahili Studies, Volume 7, Issue 1, 2024
Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.7.1.2301




**East African Journal of Swahili Studies**
eajss.eanso.org
**Volume 7, Issue 1, 2024**
**Print ISSN: 2707-3467 | Online ISSN: 2707-3475**
Title DOI: https://doi.org/10.37284/2707-3475

EANSO
EAST AFRICAN NATURE & SCIENCE ORGANIZATION

*Original Article*

# Uchanganuzi wa Mikakati ya Lugha katika Diskosi ya Kigaidi katika Magazeti ya Kenya na ya Kimataifa

*Gichohi M. Kiguta[1*], Ogola J. Onyango[1] na Wandera S. Simwa[1]*

[1] Chuo Kikuu cha Laikipia, S.L.P 1100 – 20300 Nyahururu, Kenya.
[*] Barua pepe ya mawasiliano: mchlkiguta@yahoo.com

**DOI ya Nakala: https://doi.org/10.37284/jammk.7.1.2301**

**Tarehe ya Uchapishaji:**

*14 Oktoba 2024*

**Istilahi Muhimu**:

*Mikakati, Ugaidi, Magazeti, Kenya, Kimataifa.*

**IKISIRI**

Utafiti huu ulinuiwa kuchanganulia mikakati ya lugha katika diskosi ya kigaidi kama ilivyotumiwa katika mashambulizi ya kigaidi kati ya kundi la Al-Shabaab dhidi ya serikali ya Kenya na kuripotiwa na wanahabari. Sababu kuu ya kuteua kipindi hiki ni kwamba Serikali ya Kenya na raia wake wameendelea kushuhudia mashambulizi mengi ya ugaidi ambayo yamesababisha kuzuke diskosi ya ugaidi iliyojikita katika ubishi wa kundi la ugaidi dhidi ya serikali ya Kenya. Ili kupata data ya uchanganuzi, utafiti huu ulihusu uteuzi wa diskosi ya kigaidi kupitia mashambulizi mawili makuu yaliyofanyika nchini Kenya katika duka la kibiashara la West Gate Mall mjini Nairobi na shambulio la kigaidi katika Chuo Kikuu cha Garissa mwezi wa Aprili, 2015. Kikundi lengwa kiliteuliwa kutokana na magazeti ya Daily Nation na The Standard yaliyohusu kipindi hicho cha kihistoria. Gazeti la NewYork Times liliteuliwa kutokana na upana wa mkabala wake wa mtazamo wa kimataifa. Jumla ya magazeti 145 yalikusanywa na nakala 102 zikateuliwa za mwanzoni mwa kipindi cha miezi miwili kabla na baada ya mwaka 2013-2015. Utafiti huu uliongozwa na nadharia mbili, ambazo ni nadharia msingi wa Diskosi Mkabala wa Historia ya Wodak iliyotumiwa kuchanganulia mkakati wa lugha katika vitengo vya unominishaji, urejelezi, ubishi, mkabala, uzidishaji na ufifizaji. Uchanganuzi wa mikakati ya lugha ulihusu matumizi ya kijazanda, semi, virai, vishazi na sentensi. Matokeo ya utafiti huu yalibainisha kuwa kulikuwako na tofauti za kimkabala zilizozua diskosi ya ubishi kati ya kundi la kigaidi dhidi ya serikali ya Kenya. Tofauti hizi zilibainishwa kupitia mikakati ya lugha na itikadi kutokana na mashambulizi ya ugaidi yaliyotekelezwa nchini Kenya.

**APA CITATION**

Kiguta, G. M., Onyango, O. J. & Simwa, W. S. (2024). Uchanganuzi wa Mikakati ya Lugha katika Diskosi ya Kigaidi katika Magazeti ya Kenya na ya Kimataifa. *East African Journal of Swahili Studies*, *7*(1), 463-476. https://doi.org/10.37284/jammk.7.1.2301.

**CHICAGO CITATION**

Kiguta, Gichohi M., Ogola J. Onyango and Wandera S. Simwa. 2024. "Uchanganuzi wa Mikakati ya Lugha katika Diskosi ya Kigaidi katika Magazeti ya Kenya na ya Kimataifa". *East African Journal of Swahili Studies* 7 (1), 463-476. https://doi.org/10.37284/jammk.7.1.2301

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.7.1.2301

**HARVARD CITATION**

Kiguta, G. M., Onyango, O. J. & Simwa, W. S. (2024) "Uchanganuzi wa Mikakati ya Lugha katika Diskosi ya Kigaidi katika Magazeti ya Kenya na ya Kimataifa", *East African Journal of Swahili Studies*, 7(1), pp. 463-476. doi: 10.37284/jammk.7.1.2301

**IEEE CITATION**

G. M. Kiguta, O. J. Onyango & W. S. Simwa "Uchanganuzi wa Mikakati ya Lugha katika Diskosi ya Kigaidi katika Magazeti ya Kenya na ya Kimataifa", *EAJSS*, vol. 7, no. 1, pp. 463-476, Oct. 2024.

**MLA CITATION**

Kiguta, Gichohi M., Ogola J. Onyango & Wandera S. Simwa. "Uchanganuzi wa Mikakati ya Lugha katika Diskosi ya Kigaidi katika Magazeti ya Kenya na ya Kimataifa". *East African Journal of Swahili Studies*, Vol. 7, no. 1, Oct. 2024, pp. 463-476, doi:10.37284/jammk.7.1.2301.

## UTANGULIZI

Diskosi ya ugaidi imeendelea kuwa swala sugu katika kila pembe ya ulimwengu. Hii ni kutokana na sababu ya kuwa magaidi wameendelea kuzua hofu, vitisho na woga kwa wanajamii. Ni bayana kuwa ugaidi umeendelea kuibua mitazamo tofauti ya kimkabala, kimikakati na kimatumizi jambo ambalo limeendelea kuzua ubishi katika makundi ya kijamii. Kila kundi huliona mwenzake kutokana na mitazamo tofauti iliyojikita katika itikadi. Ubishi katika muktadha wa diskosi ya ugaidi kupitia kundi la Al-Shabaab dhidi ya serikali ya Kenya na kimtaifa kupitia mashambulizi ya Westgate (2013) na Chuo kikuu cha Garissa (2015) unahitaji kuchanganuliwa kwa kina kupitia mwafaka mahsusi wa kinadharia. Utafiti huu ulinuia kuliziba pengo hilo la kiusomi. Magaidi hunuia kuelekeza shabaha yake katika maeneo na makusanyiko makubwa ya halaiki ya watu, kama vile: majumba ya burudani, maduka makubwa ya kibiashara na majumba ya ibada (Exposito, 2002). Magaidi hulenga kusababisha hasara, hofu na woga kimaksudi ili kujinufaisha kisiasa na kiitikadi (Anwar, 2009).

Ugaidi si jambo geni katika maisha ya binadamu (Jowett & O'Donell, 2006). Usababishaji wa vita vya kikatili na uzuaji vurugu dhidi ya wanajamii ni mbinu ambazo zimekuwa zikitumiwa kama mkakati wa ubishi katika mapambano ya kijamii kati ya makundi ya magaidi na mataifa mbalimbali (Friedlander, 1976). Historia ya ugaidi ilishuhudiwa vyema katika karne ya 18 katika vita vya mapambano ya kimapinduzi nchini Ufaransa, katika kipindi cha kihistoria nchini Ufaransa kilichojulikana kama kipindi cha utawala wa udhalimu na kimabavu (Hansen, 2013). Vita hivyo vya kimapinduzi vijulikanavyo kama French Revolution vilishuhudiwa kati ya Septemba 5, 1793 hadi Julai, 27, 1794 wakati serikali ya Ufaransa iliandikisha sheria kali dhidi ya raia yeyote ambaye angepatikana akitenda mambo kinyume na maagizo ya utawala wa serikali wa nyakati hizo. Raia wa Ufaransa waligomea utawala wa kimabavu wa Napoleon katika peninsula ya Uhispania ambapo kulichipuka mtindo mpya wa upiganiaji ambao ulijulikana kama 'guerilla'.

Mtindo huu ulihusu wanamgambo kujificha kisha kushambulia majeshi tawala kwa mshtukizo. Hapo ndipo neno 'guerilla' lilichipuliwa ambapo lilitokana na neno la kihispania 'guerra' na lililomaanisha vita vidogo (Friedlander, 1976). Kimataifa, ugaidi ulikuja kufahamika vyema kimaana na kimatumizi hasa katika karne ya kumi na tisa na kufikia kileleni chake mwaka wa 1970 katika vita vya troubles wakati mbinu mpya kama vile za kujitoa uhai zilipoanza kutumiwa na magaidi katika Kisiwa cha Kaskazini (Northern Island) na katika mgogoro nchini Blasko (the Blasque Conflict) na pia katika mgogoro wa kivita dhidi ya Waisiraeli na Wapalestina (Israeli-Palestina Conflict). Baada ya mwaka ya 1990 ndipo mashambulizi ya ujitoaji uhai kupitia vilipuzi na utekaji nyara kupitia ndege zilianza kushika kani Marekani mwezi wa Septemba 11, 2001 katika vita vya ugaidi vilivyowahi kuwa vikubwa zaidi ulimwenguni. Vitendo vya kigaidi ni pamoja na utekaji nyara, ulipuaji wa majengo na kusababisha mauaji palipo na makusanyiko wya watu (Halliday, 1996). Lengo kuu la ugaidi ni kusababisha hofu na hasara kubwa iwezekanavyo (Hiro, 2002).

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.7.1.2301

Wafuasi wa ugaidi wanaamini kwamba mashambulizi ni mkakati wa ubishi wa kuvutia umakini wa mkabala wa madai yao ili kupata suluhisho litakalofaidi maslahi na itikadi zao. Kwa wakati huu, matendo ya kigaidi yanashuhudiwa kwa wingi katika maeneo ya Israeli, Iraq, Indonesia, Uingereza, Sri-lanka, Colombia, Syria, Marekani, Afrika Magharibi na Mashariki (Hoffman, 2006). Ugaidi wa kimataifa uliokuwa mkubwa zaidi kushuhudiwa, ulifanyika Marekani mwezi wa Septemba 11, 2001 na uliongozwa na kiongozi wa Al-Qaeda Osama bin Laden. Ugaidi huu ulihusu mashambulizi ya kujitolea mhanga na uhai na utekaji nyara wa ndege na ulipuaji majumba (Lacquer, 2001). Asubuhi hiyo ya 9/11, magaidi kumi na tisa walivamia ndege nne za kibiashara zilizotarajiwa kusafiri kutoka New England na Atlantiki ya Kati (Mid-Atlantic) ya sehemu za maeneo ya pwani ya magharibi (East Coast) kuelekea California. Matendo ya ugaidi kupitia Al-Qaeda yalikuwa yameshuhudiwa mwanzoni zaidi (Ditrych, 2014) katika vita vya Urusi nchini Afghanistan. Umoja wa Marekani ulichukulia vita nchini Afghanistan, vya Allied Marxists na askari wa Urusi upande mmoja na raia wa Afghanistan wa mujahideen upande wa pili, kama kesi ya unyakuzi wa mipaka (Abdisaid, 2008).

Magaidi hao wa kundi la Al-Qaeda walilipua ndege mbili za kwanza kwenye Twin Towers ya jumba la World Trade Centre huko mjini New York ambalo lilikuwa na majengo mengine matano yaliyokuwa marefu zaidi duniani wakati huo (La Free, 2014). Katika mashambulizi hayo, ndege ya tatu kati ya zile zilizokuwa zimetekwa nyara na magaidi ilielekezwa kulipua maeneo ya Washington DC na Pentagon ambayo yalikuwa makao makuu ya ulinzi Marekani yaliyoongozwa na US Department of Defense katika kaunti ya Arlington, Virginia. Ndege ya nne ilielekezwa kulipua makao makuu ya jumba la kiserikali katika mji mkuu wa Washington DC lakini ikakosa mwelekeo kutokana na abiria waliokuwemo ambao walipambana na magaidi na ilielekezwa katika vitongoji vya Pennyslavania na kulipuka. Mashambulizi haya ya kigaidi yalisababisha vifo vya jumla ya raia 3000, maelfu ya watu walijeruhiwa vibaya na wengine wakapata majeraha yaliyosababisha matatizo ya kiafya.

Ni bayana kuwa katika mashambulizi ya ugaidi kila kundi lilitumia lugha kama mkakati wa ubishi kuelezea mkabala wake (Lacquer, 2001). Makundi yanayobishana yalitumia maneno ya kutetea msimamo wake uliojikita katika itikadi (Goodin, 2006) ili kujaribu kulishawishi kundi pinzani kuzingatia mtazamo wake. Maneno kuhusu kauli za vitisho na uzuaji hofu yaliteuliwa na magaidi kutelea matangazo ya mashambulizi ya ugaidi na pia kama mkakati wa nguvu katika mjadala wa diskosi ya ugaidi (Hiro, 2002). Mkakati wa vitisho uliandamana na utumizi wa propaganda, chuku na upotoshi ili kuongezea nguvu ya mawasiliano (Schmind, 1988).

## MAPITIO YA MAANDISHI

Wodak (1995) anaeleza kuwa mkakati wa diskosi ni mbinu za mawasiliano zinazotumiwa katika lugha katika muktadha wa wanajamii. Ni jinsi wanajamii hutumia maneno katika mawasiliano ili kuathiri jambo (Van Dijk, 2001, 2008). Huhusu mbinu za lugha zinazotumiwa na msemaji ili kumtaka mnenewa awe makini kuhusu muktadha wa ujumbe unaopashwa (Blommaert, 2005). Lugha hutumiwa kama chombo muhimu katika ugomvi wa makundi (Woods, 2013).Lugha hutumiwa katika ukuzaji wa mgogoro na pia katika kuusuluhisha (Walton 1998; Woods, 2013 na Eemeren, 1999). Mkakati wa lugha ni muhimu katika ujenzi wa ubishi ambapo kila kikundi hujibidiisha kudidimiza mwenzake katika mashindano ya mjadala mkali unaofungamana na itikadi.

Magaidi hutumia maneno ya kushawishi au kushinikiza ili wapate kufaidika kutokana na madai yaliyotolewa (Schmind, 2005). Miundo ya maneno katika sentensi, vishazi , virai na maana huashiria dhana mbalimbali zilizotolewa (Ross, 2006). Diskosi ya ugaidi ilihusika katika mkakati wa lugha uliodhamiriwa kutumia nguvu katika malumbano ya magaidi dhidi ya serikali katika mashambulizi ya ugaidi (Odhiambo, 2014). Kundi la kigaidi lilitekeleza mashambulizi kwa

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.7.1.2301

ishara ya kuonyesha uwezo wake wa kivita na uwezekano wa kuyaendeleza mashambulizi iwapo madai yake hayangeshughulikiwa ipasavyo na serikali (Miller, 2004; Stanley, 2002). Mikakati ya usababishaji wa uharibifu, mauaji na vitisho ilisaidia Al-Shabaab katika mapambano ya nguvu dhidi ya serikali (Van dijk, 2001, 2006; Wodak na Meyer, 2001). Vitengo mbalimbali vya lugha vilitumiwa katika utangazaji woga na vitisho kama vile: kushawishi, kukashifu, kujenga uaminifu, kujenga mgogoro, kuathiri hisi, kupotosha, kujisifu, kutangaza vita, kutolea hoja, kupinga hoja, kudai, kulalamika, kuapiza, kulaumu, kukashifu kama mkakati na mbinu za ujenzi wa ubishi na pia maneno hayo yalitumiwa kama silaha ya nguvu ya ushindani wa kisiasa (English, 2009). Wodak (2008) alieleza kuwa mkakati ya diskosi ya usemi ulihusu mpangilio wa matumizi ya lugha kupitia kategoria. Mkakati wa diskosi ulijadili jinsi mtu hupewa sifa na jina, na jinsi wanajamii na vikundi mbalimbali hutumia lugha katika mahusiano. Njia mojawapo ya jinsi makundi ya kijamii hushindana kupitia mkakati wa nguvu ya usemi kati ya mnenaji na mlengwa wake kupitia matumizi ya lugha katika muktadha (Wodak, 2001).

Kupitia *toposi*, mtafiti alibaini jinsi makundi ya wanajamii katika mgogoro yalivyotumia ala za mikakati ili kushawiashi matokeo au katika malumbano ya usemaji wa lugha kiufasaha (Ryszard, 2011). Aristotle, kupitia maelezo ya Frost (2005) kama mwanzilishi wa dhana ya toposi alielezea kuwa ilikuwa ni muhimu kufahamu nafasi ya mhusika katika malumbano. Chanzo cha mgogoro alikuwa ni ‘msemaji wa maneno’ au ‘mwandishi’ aliyechukua nafasi na msimamo wa kuanzisha malumbano ya mada husika. Kwa kurejelea msingi huu kama kielelezo, mwanzilishi wa usemi katika malumbano ya ugaidi alikuwa ni Al-Shabaab (*Daily Nation*, 2013-2015; *The Standard*, 2013-2015 na *NewYork Times*, 2013-2015). Al-Shabaab walitumia mkakati wa maneno ya vitisho dhidi ya serikali ya Kenya. Maneno ya Al-Shabaab yalijikita katika msimamo wa kiitikadi ili kuzindua kauli za mgogoro. Kwa upande mwingine, serikali ya Kenya pamoja na wanahabari wakiongozwa na mkabala walitumia maneno teule ili kupasha habari kwa hadhira na kuchukuliwa kuwa walikuwa wakipinga yaliyotolewa kutokana na itikadi tofauti (Lawyer et al., 2014). Fairclough (2003) na Ditrych (2014) wanaeleza kuwa majadiliano ya kijamii yanaweza kuongozwa na vigezo vitatu vya mkakati wa topoi ambavyo ni -mienendo, mpangilio wa mantiki na maadili.

Kupitia mienendo ya topoi makundi yalitathminiwa kufuatia matumizi ya maneno yaliyohusiana na ushawishi wa kihisia kwa raia kutokana na sababu ya kuwa na madharau, makasiriko, ubaguzi au kutengwa, uvurugaji, na sababu ya kuchukua hatua ya haraka, sababu za kuzidisha mipaka ya matendo yaliyotukia na sababu ya kuanzisha vita vya kighafla. Mpangilio wa mantiki katika upashaji habari kwa wanajamii katika makundi ulihusu kuchunguza jinsi mikakati ya matumizi ya maneno yalivyotumiwa kwa miundo kama vile virai, vishazi, ukweli dhidi ya upotoshi, ukubalifu wa maneno katika muktadha. Maadili katika topoi (Huhtamo, 2011), yalihusu kutathmini jinsi makundi yaliweza kutumia maneno yenye vishawishi vikubwa kwa wanajamii kwa kutumia maneno yanayoibua uzalendo, imani, desturi, utamaduni (haki, usawa, umoja, utaifa,kiasi, uvumilivu na subira, kutokujali, ushirikiano, kumcha Mungu, na usemaji ukweli au uongo), na tabia (Sharples, 2001). Vigezo hivi vya matumizi ya lugha kwa topoi (Obrecht-Tyteca na Rerelma, 1982) vilibainisha makundi hayo ili kufahamu walengwa katika matumizi ya lugha na lengo la kuchuklua hatua ambayo ilichukuliwa (Ryszard, 2011).

Kundi la kigaidi lilipinga na kukashifu mkabala wa itikadi za serikali ya Kenya nayo serikali ya Kenya vile vile ilipinga mkabala na mikakati iliyotolewa na kundi la ugaidi. Utafiti huu ulitumia lugha ya wanahabari kupitia magazeti. Utafiti uliweza kubainisha jinsi kundi moja lilivyoweza kulipa kundi lingine jina kwa kulitambulisha na kulirejelea kundi hilo. Kundi la kigaidi la Al-Shabaab lilihusishwa na ishara za vita, mauaji, dhulma/ ukatili, uharibifu, ukosefu

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.


Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.7.1.2301

wa usalama na mateso. Kundi la Al-Shabaab kwa upande wake liliona serikali ya Kenya kama inayojihusisha na ubaguzi na kutenga baadhi ya makundi, kuingilia maisha ya wanajamii kwa majigambo. Kila mojawapo ya kundi lilishikia msimamo wake hali iliyozua mtafaruku wa ushindani katika matumizi ya lugha (Jackson, 2016). Wodak (2001) anaeleza kuwa diskosi ya usemi iliweza kuchanganuliwa kupitia mihimili mitano mahsusi ambayo ni: Urejelezi, unominishaji, ubishi, mkabala, uzidishaji na ufifizaji. Mkakati wa unominishaji ulitumiwa kujadili jinsi makundi ya kijamii katika mapambano ya kisiasa yalivyoashiriwa.

Kwa mfano kundi la kijamii lilipewa majina yaliyorejelea sifa nzuri zilizobashiri matendo yao kama vile:*wapiganiaji utu na ubinadamu*, *wazalendo watukufu*, *raia wapenda haki*, *raia wenye utu* ilihali maneno yaliyoelekezewa magaidi yaliashiria kudidimiza matendo yao kwa mfano *wabinafsi*, *watu wasio huruma*, *wasiopenda haki*, *wakatili*, *wamwagaji damu isiyo kuwa na hatia*, *wauaji*, *wasaliti*, *wadhalimu/wakatili*. Mkakati wa urejelezi (Wodak, 2001) ulitumiwa kubashiri matokeo ya mahusiano kati ya makundi ya kigaidi ya Al-Shabaab na serikali ya Kenya kupitia mielekeo, mitazamo na itikadi. Mkakati wa ubishi (Wodak, 2001) ulikuwa muhimu katika kuchanganulia maneno yaliyolenga kukuza hoja za kutetea mjadala. Hoja zenye kauli za kweli na za upotoshi zilibainishwa kupitia mnenaji (Kress na Hodge, 1979). Maneno ya mneneji yalichunguzwa jinsi yalivyoongozwa na kujikita kwenye itikadi, mielekeo na misimamo ya ushahidi kuhusu matendo yaliyotendwa na kundi moja dhidi ya lingine.

Mtafiti Van Eemeren na Grotendorst (1992) alichunguza jinsi ubishi ulivyojengwa katika malumbano ya kijamii. Mtafiti aliteua maneno katika muktadha yaliyojenga ukinzani kwenye matini ya magazeti. Maneno yalitumiwa kama data ya uchanganuzi yalihusu mikakati ya usemi wa makundi kama vile, kauli potoshi (Walton, 1995), za propaganda (Van Dijk, 2006), kauli za vitenzi- neni (Searle, 2005) kama vile : vitisho na hujuma, hisia za chuki na dhihaka, za kejeli na mabezo. Kauli hizi zililinganishwa na kauli za kuaminika zenye mantiki. Yazdan (2016) anaeleza kuwa diskosi ya ubishi ilikuwa muhimu katika ujenzi wa mgogoro kati ya makundi ya kijamii. Ubishi ulitumiwa kuchunguza tofauti ya mikabala na mitazamo ya itikadi kati ya makundi iliyofanya kuwe na mashindano katika usemi. Toulmin (1950) anafafanua ubishi kwa kutumia misingi mitano ya ujenzi wa midahalo ya ukinzani. Misingi hii ya ubishi iliweza kugawanywa katika vigezo vya madai, data zilizotolewa, ukubalifu, dhihirisho na mantiki. Kulingana na maelezo ya Toulmin, 1950 na Eemeren, 2014, kila ubishi huanzia kwa vijisehemu vitatu vikuu ambavyo ni madai, dhihirisho na mantiki.

**Jedwali 1: Kielelezo Kuhusu Vitengo vya Ujenzi wa Ubishi (Toulmin, 1950)**




Madai ni mada ambayo iliyoongoza mjadala kama kisababishi na chanzo kuu inayotambulisha mgogoro (Walton, 2013). Dhihirisho ni ushahidi unaotolewa kuunga mkono au kuthibitisha madai

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.7.1.2301

yaliyotolewa na mantiki ni yale mambo ambayo yaliyoshukiwa kutokana na madai yaliyotolewa (Walton, 1998). Johnson (2000) alijadili jinsi ubishi ulivyodhihirika katika makundi mawili ya kijamii. Kwa kupitia msingi wa nadharia ya ubishi, alieleza kuwa ubishi ni mojawapo ya mada changamano iliyofungamana na mada zingine anuwai (Tazama Jedwali 1). Hii ni kwa sababu nadharia ya ubishi (Walton, 2013) ilichunguza jinsi makundi yalivyopambana katika mgogoro kila kundi likitetea upande wake na kujaribu kupata suluhisho ua maafikiano yenye urazini ufaao na wakati mwingine suluhu haikupatikana kabisa wakati kila mojawapo wa kundi lilisimamia mkabala wa ‘ukweli’ wa upande wake. Van Eemeren na Grootendorst (1992) walifafanua nadharia ya ubishi kuwa iliweza kutumiwa kama nguzo kuu katika uchanganuzi wa malumbano. Nadharia ya ubishi ilitumiwa kutathmini na kuweka kwa mizani madai yaliyotolewa na kundi moja dhidi ya lingine (Van Eemeren et al., 2002).

Nadharia ya ubishi ilitumiwa pia kutadhimini kama hoja zilizojadiliwa zilikuwa na ukubalifu na ukweli au zilibeba udanganyifu na kutoaminika (Woods, 2013). Nadharia ya ubishi ilikadiria hoja zenye ushawishi mkubwa kuliko zingine au zinazopotosha madai yaliyotolewa (Walton, 2013). Nadharia ya ubishi ilichunguza mkakati wa usemi uliotumiwa na kundi moja katika mdahalo kulishurutisha lingine likubali kufuata mkondo wake (Eemeren, 2014). Walton (2013, 2015), anaeleza kuwa ubishi katika malumbano ulijengwa kupitia umbo la vigezo vitatu vikuu ambavyo ni: i) Utangulizi ii) Masimulizi na iii) Ufafanuzi. Mtafiti alichanganua kauli za madai zilizotolewa na makundi mawili ya kijamii yenye mgogoro na kutathmini zile zilizokuwa za kweli na uhakika dhidi ya zile zilitiliwa shaka au potoshi katika malumbano. Mtafiti aliongozwa na uhakiki wa nguzo zifuatazo za nadharia ya ubishi:kutathmini maeneo ambapo suluhu ilipatikana ili kuafikiana katika mgogoro (Eemeren, 2014), kutathmini ushahidi uliotolewa na mnenaji kumshurutisha mlengwa kuchukua hatua ya matendo yake (Walton, 2013), kutathmini matumizi hoja za nguvu zilizotolewa kumshawishi mlengwa kukubali hoja zilizotolewa. (Eemeren & Grotendorst, 1992) Kutathmini mada kuu katika mjadala iliyobainisha kuwa na mikabala tofauti katika makundi (Ryan na Bernard, 2013).

Blair na Ralph (1997) walijadili umbo ndani la ubishi kuwa huwa na vipengele vifuatavyo:Madai yanayotolewa, Mpangilio wa kukuza hoja za kweli au potoshi, Suluhisho na maafikiano. Mkakati ya ubishi huwa na suluhisho moja ambalo hufikiwa ingawa fikira au hoja zinaweza kuwa zaidi ya moja (Van Eemeren na Grotendorst, 1992). Mataifa mbalimbali yalichukulia kundi la Al-Shabaab kama kundi lisilozingatia haki za kibinadamu na lenye malengo ya kusababisha hasara duniani kupitia vitisho na mauaji (Walzer, 2004). Kupitia mtazamo wa Al-Shabaab dhidi ya serikali ya Kenya na mataifa ya ulimwengu ni kuwa lilikuwa likibaguliwa na kudunishwa na kwa hivyo lilihitaji mikakati ya kupambana na kutangaza msimamo wake kupitia itikadi (Vito D’orazio, 2018). Hali hii ndiyo chanzo cha ubishi kupitia mikabala tofauti ya kimsimamo kati ya kundi la Al-Shabaab kwa upande mmoja dhidi ya serikali ya Kenya na za Kimataifa (Odhiambo, 2014). Kila kundi liliongozwa na msimamo wake uliojikita katika itikadi (Schmid, 2005).

Kila kundi lilibandika mwenzake lebo la ugaidi kutegemea mtazamo aliouona kwa kundi pinzani (Boru, 2004; Cole, 2003). Katika ujenzi wa mgogoro wa ubishi kati ya makundi haya, serikali hutumia mkakati wa maneno ya kuonyesha kuwa matendo ya magaidi yalikiuka haki na usawa wa kibinadamu na magaidi kwa upande wao hujitetea kuwa serikali zinatumia majeshi yao vibaya kwa kuwadhulumu magaidi na kuingilia maslahi yao ya kindani (Van Dijk, 2000).

Mtazamo wa Al-Shabaab ni kuwa Kenya na mataifa ya ulimwengu zilitumia mbinu za kigaidi kuvamia maswala yake ya kindani na uongozi wake (Toomey na Singleton, 2014). Kwa upande wa pili, nchi ya Kenya na za kimataifa zilichukulia kuwa hatua zilizochukuliwa na Al-Shabaab za vitisho na mashambulizi zilikuwa za kigaidi na zilikiuka haki za kibinadamu (Russel na Tyler,

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.7.1.2301

2010). Al-Shabaab na makundi mengine yalichukulia kuwa neno 'gaidi' lilitumiwa na nchi za kimataifa kutambulisha na kudidimiza makundi madogo yaliyojaribu kujitetea (Lacquer, 2001). Kundi la Al-Shabaab liliendelea kupigana na huchukuliwa kama maadui wa Uislamu katika Somalia, Kenya na Yemen. Higgins na wengine (2017) wanaeleza kuwa Al-Shabaab lilitumia mkakati wa itikadi ya tadmini inayohusu manukuu ya maandishi maarufu kutoka kwenye kurani na kuyageuza ili kutumia kama hoja kali za kutetea mashambuzi waliyosababisha. Al-Shabaab lilitumia dini ya Kiislamu kutilia shaka na kutoaminiana kati ya waislamu wa Kenya na Somalia (Abdisaid, 2008).

Baadhi ya Wakenya huwachukulia Waislamu kama Al-Shabaab kutokana na itikadi za dini ya uislamu zilizofanganishwa na Al-shabaab (Abdi, 2023). Kupitia unyanyapaa wa kuhusisha uislamu na ugaidi, baadhi ya wakenya wamekuwa wakiwatambulisha Wasomali kuwa ni Al-Shabaab (Anwar, 2009). Serikali ya Kenya na Somalia zimekuwa na changamoto kubwa ya kubainisha Waislamu halisi wa Somalia na wale wa kundi la Al-Shabaab (Ahmad, 1977). Fischer (2004) anaeleza kuwa ubishi hutumiwa kupanga hoja mbalimbali za kugeuza mtazamo wa mpinzani ili aweze kukubali kuunga mkono mtazamo wa mnenaji. Lengo kuu la mnenaji katika malumbano huwa ni kushawishi mpinzani wake akubali kuona upande wa maoni yake kupitia ushahidi uliotolewa wa maneno (Eemeren, 2014). Mnenaji hutoa ushahidi wa kweli au uongo kutokana na imani anazozisadiki na kuzifuata (Walton, 1998). Utafiti huu ulichunguza mkabala wa kundi la Al-Shabaab na hoja ilizotoa katika malumbano dhidi ya mkabala wa serikali ya Kenya na kimataifa na jinsi kila mojawapo wa kundi lilivyoongozwa na msimamo wa itikadi zake kutolea ushahidi mkali wa kujitetea. Ushahidi wa mneneji uliweza kutolewa kupitia jambo la wazi au la maoni (Van Eemereng, 2009). Jambo hilo la wazi liliweza kukadiriwa kupitia mfumo wa kisayansi kufikia uamuzi uliokubalika kihalali (Woods, 2013). Utafiti huu ulichanganua jinsi mkabala wa wanahabari kuhusu ugaidi ulivyoweza kuathiri matangazo kufikia wanajamii kuhalali au kupotosha ujumbe.

Habari iliyopokelewa na hadhira lengwa kuhusu matangazo ya ugaidi kupitia magazeti zilitawaliwa na mkabala wa wanahabari. Wanahabari kama zao la kijamii waliongozwa na mkabala wa serikali zao walizohudumia au mkabala mpana wa kilimwengu kuhusu ugaidi (Van Dijk, 2000, 2006). Lengo la utafiti huu lilikuwa ni kuchanganua diskosi ya kigaidi kupitia taaluma ya kiusomi ( Wodak na Krzyz'anowski, 2008) kupitia mkabala wa makundi ya ugaidi dhidi ya serikali ya Kenya na ya kimataifa, kutathmini mikakati ya lugha (Wodak , 2001) katika matini ya magazeti ilivyotumiwa kuzua malumbano ya ubishi (Eemeren & Grotendorst, 1992). Ubishi uliweza kubainika kutoka na jinsi makundi mawili yalivyoongozwa na misimamo mikali ilivyojikita kwenye itikadi (Eemeren et al., 2002).

Mkakati wa mkabala ulitumiwa kuchunguza jinsi baadhi ya makundi ya kijamii yalitumia maneno ya kutenga na kubagua kundi pinzani kwa kulishusha hadhi kupitia matumizi ya lugha (Van Dijk, 2008). Kundi moja lilitumia maneno na ishara za kulemaza kundi lingine ili lionekane dhaifu mbele ya wanajamii (Wodak, 2001). Itikadi zinazoongoza kundi hilo zilipuuzwa na kukashifiwa kuwa hazikufaa (Van Dijk, 1984). Mkakati wa ubaguaji ulihusu uteuzi wa maneno yaliyoonyesha utengaji wa kundi moja kuwa la 'Wao' na kupendelea "Sisi" (Reisigl &Wodak, 2001).

Nakala za magazeti zilizoteuliwa zilionyesha mkabala unaohusu ubaguaji wa kundi moja dhidi ya lingine kupitia kauli za dharau au bezo, majigambo, kejeli, kukashifu, kulaumu, kuapiza kutokana na misimamo na mitazamo (Wodak, 2001). Mkakati wa ubaguzi ulichunguza jinsi makundi ya kijamii hushindana katika malumbano ya lugha kuhusu ubaguaji na upuuzwaji wa kundi lingine (Ricouer, 1992). Mkakati wa uzidishaji na ufifizaji wa matumizi ya maneno kati ya kundi moja la kijamii dhidi ya lingine ulichunguza ripoti za wanahabari. Mkakati huu ulikuwa muhimu kutathmini ethnografia ya

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.7.1.2301

usemi kuhusu kauli za kundi moja zilivyotumia maneno ya kuzidishia na kutilia chuku pamoja na propaganda kujitukuza huku likididimiza lingine katika muktadha wa mawasiliano (Miller, 2004; Michael, 2005; Van Dijk, 2006).

Utafiti huu ulitathmini maneno yalivyoongozwa na itikadi (Yazdan, 2016) kujieleza na kueleza kundi pinzani. Chomsky (2004) anaeleza kuwa mkakati wa propaganda (Van Dijk, 2006) ulitumiwa kubainisha kauli zilizoonekana za kweli au zile zilizopotosha ukweli kwa kuzidisha, kudanganya, kutilia chuku au kufifiza habari ziwe na nguvu au zikose nguvu katika mawasiliano. Maneno yaliyoteuliwa kutoka kwa matini ya magazeti yalihusu semi na jazanda zilizozidisha au kudhoofisha matumizi ya maneno (Van Dijk, 2006). Baadhi ya maneno yalitumia kauli za ukali kutoka kwa mnenaji hadi kwa mpokeaji (Van Dijk, 1991, Reah, 2002). Uandishi wa magazeti ulihusu makala kulingana na maoni ya mkabala wa kundi lingine ( Van Dijk, 2008).

Maneno ya wanahabari yaliongozwa na mkabala uliofifiza au kuongeza kauli zilizotolewa kutegemea mkabala wa umma (Rutherford, 2000). Kwa kuchunguza mkabala wa magaidi kwa upande mmoja, na mkabala wa serikali na mkabala wa wanahabari, mtafiti alitathmini jinsi makundi yalivyoongozwa na itikadi (Van Dijk, 2000 na 2001) zilivyohusiana na kuzua malumbano ya ubishi.

**Mkakati wa Diskosi ya Ugaidi**

| **Mkakati wa usemi** | **Mada za usemi** | **Malengo** |
|---|---|---|
| Mkakati wa Urejelezi | Mitazamo, mielekeo, imani na itikadi zinazohusishwa na kurejelewa na sifa za wahusika. | Kutathmini jinsi sifa chanya au hasi za maneno zinavyohusishwa na matendo ya kundi fulani la kijamii . |
| Mkakati wa Unominishaji | Jinsi mtu ,watu au makundi ya watu katika jamii yanavyosawiriwa. | Kutathmini na kutoa arifa za jinsi, mtu au watu walivyohusishwa na ishara za majina ya matendo na matukio yao kupitia mtazamo wa kundi moja la kijamii dhidi ya lingine |
| Mkakati ya ubishi | Mikinzano na midahalo ya lugha inayoandamana na itikadi na imani za wahusika. | Kutathmini maneno yalivyotumiwa katika malumbano ya kisiasa na kijamii na kundi moja dhidi ya lingine kupitia itikadi, mielekeo na mitazamo. |
| Mkakati wa Mkabala | Migogoro inayotokana na mkabala wa ubaguzi wa kidini, kitabaka, kiuchumi na kimtazamo | Kutathmini jinsi mnenaji anavyotumia maneno au kauli zinazomdhalilisha au kumdunisha mwenzake katika kundi pinzani ili kumpuzilia na kumfanya aonekane dhaifu akiongozwa na imani na itikadi zake. |
| Mkakati wa uzidishwaji na ufifizwaji | Maneno yalitamkwa kwa njia gani? Je, yameongezewa chumvi au chuku? Je, ni ya kweli au wameongezewa mambo ambayo si ya kweli wakati kundi moja la kijamii linaponena kuhusu kundi lingine? | Kutathmini kauli za kimkabala zinazotumiwa na kundi moja la kijamii dhidi ya lingine. Je, kundi moja linaibua matumizi ya uzushi na propaganda kulisawiri lingine kupitia itikadi na imani zake? Kundi moja linanuia kuibua hisi zipi kimtazamo wakati linaripoti kuhusu kundi pinzani la kijamii? |

**Kutoka kwa :** Wodak (2001)

Jedwali (Taz. Jedwali kuhusu mkakati wa Diskosi ya Ugaidi) linaangazia vigezo vitano vya mkakati ya diskosi vilivyotumiwa katika uchambuzi wa lugha ya ugaidi kwa mujibu wa Diskosi Mkabala

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.7.1.2301

wa Historia kubainisha vitengo vya unominishaji, urejelezi, ubishi, mkabala, uzidishaji na ufifizaji wa ujumbe. Wodak (2015) alieleza kuwa vitisho vilikuwa ni njia nyingine ya kimkakati iliyotumiwa na kundi la kigaidi kushurutisha serikali ifuate na kukubali mtazamo wake. Vitisho na woga vilikuwa ni mikakati uliohusu matumizi ya nguvu na uwezo ili kuogopewa (Abdi, 2023). Vitisho hivi viliandamana na maneno ya upotoshi au propaganda (Schmind, 1988). Vitisho ni mbinu ya kisaikolojia inayotumiwa na makundi ya kigaidi kuogopesha serikali ya Kenya na ya kimataifa kushinikiza madai yake (Oando na Ochieng, 2021).

Kwa mfano, baada ya mashambulizi ya kigaidi dhidi ya serikali ya Kenya, kundi la Al-Shabaab lilijigamba kuwa ndilo lililohusika na shambulio la *Westgate* mjini Nairobi kwa kusema *"Shambulio hili lililofanyika katika duka la Westgate ni sisi Al-Shabaab ndio tulitekeleza' Daily Nation* (2013). Kwa kutumia maneno ya viwakilishi huru kama vile *sisi* ilikuwa ni njia mojawapo ya kujirejelea na kuzitenga jamii zingine (Stanley, 2002). Makundi katika mkinzano yalitumia masimulizi ya kuonyesha uwezo walio nao ( Rutherford, 2000). Kwa mfano, wakati Waziri Mkuu wa nchi ya Canada alipokuwa akiwahutubia Wakenya baada ya shambulizi la kigaidi alitaka kuonyesha kuwa magaidi hawakuwa na uwezo mkubwa kwa kutumia maneno kuwa: *'Tunawahimiza viongozi wa Kenya kuwakamata wahalifu hao wa kigaidi, kuwashitaki na kuwatia korokoroni."(Daily Nation*, 2013)

Kwa kuwapa majina kama vile *wahalifu hao* ni njia ya kulididimiza na kulitenga kundi la kigaidi ili lionekane kuwa linahusika kwa matenda ya uhalifu na uvunjaji sheria (Friendlander, 1976). Mkakati mwingine uliotumiwa ulihusu matumizi ya maneno ya ubaguaji unaodhihirisha chuki na dharau ili kundi liweze kuchukiwa na wanajamii (Wodak, 2001). Kwa mfano, Katibu Mkuu wa Marekani alipokuwa akitoa hotuba baada ya shambulizi la ugaidi katika Chuo Kikuu cha Garissa alisema, *" Maneno pekee yake hayawezi kutosheleza hisia tulizo nazo za hasira na simanzi na matarajio yetu ni kuwa kama ingeliwezekana maisha ya wapendwa wetu hayangepotea' Usuli: The Standard* (2015). Maneno kama vile *hisia tulizo nazo* yananuiwa kulitenga kundi la Al-Shabaab kuwa ni 'Sisi' dhidi ya 'Wao' na vilevile kuteka na kuathiri hisia za hadhira lengwa. Serikali zilihusisha kundi la Al-Shabaab kwa majina yaliyoandamana na matendo yake kama; *"ya kinyama yaliyovuka mipaka ya kijamii'*.

Maneno ya *kinyama* yalitumiwa kimaksudi kutenganisha yale yaliyotekelezwa na Al-Shabaab hayakuwa ya kibinadamu (Wodak, 2001). Taswira iliyokusudiwa kwa walengwa iliwahitajiwa kuwarejelea Al-Shaabab kama viumbe waliokuwa na kasoro ya ubinadamu (Wodak, 2001). Ingawa kundi la Al-Shabaab lilijaribu kujitetea kutokana na madai yaliyotolewa, hali hii ilitumika kujenga na kukuza mgogoro na ushindani wa maneno (Unvar na Rahim, 2013). Kundi moja lilijaribu kulitawala lingine kupitia matumizi ya maneno kwa kulishusha na kufifiza hadhi ya kundi pinzani(Scollon, 1998). Al-Shabaab ilikuwa ikishirikiana na makundi mengine ya uislamu yaliyokuwa na itikadi za mrengo wa *kijihad* kama mkakati ( Abdisaid, 2008).

Baadhi ya makundi yaliyohusiana na Al-Shabaab ni kama vile : Qutbist, Salafist, Sunni, Takfiri, Wahhabi na Al-Qaeda ( Jackson, 2014; Rohan, 2005; Mouna, 2021). Kress (1985) walieleza kuwa kipengele cha lugha kilikuwa chombo cha mawasiliano katika diskosi ya ugaidi. Lugha ilitumiwa katika nyanja ya utawala na mgogoro (Fowler, 1979), katika midahalo ya siasa na ushindani kati ya makundi na kuweka wazi mahusiano ya kimakundi (Fairclough, 1989). Lugha ilitumiwa kama chombo cha kudhulumu, maonevu, na ubaguzi (Bourdieu, 1991).

## MATOKEO

Ni dhahiri kuwa mikakati ya diskosi ya lugha ya ugaidi ilitumika katika diskosi ya ugaidi kukuza ubishi kati ya kundi la Al-Shabaab dhidi ya serikali ya Kenya na kimataifa. Matumizi ya lugha ilizua midahalo ya ubishi kupitia vitenzi neno vya kudai haki, kuhusisha matendo, kubagua

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.7.1.2301

na kufifiza, kujitukuza na kujipa sifa, kushawishi, kuapiza na kulaumu na vile vile kuzingatia kiwango kilichofaa katika unenaji. Mikakati ya diskosi ya lugha katika mjadala wa ugaidi ulitumiwa na makundi ya kijamii. Mikakati mitano ya kidiskosi (Wodak, 1909) ilijadiliwa. Mikakati hii ni urejelezi, unaominishaji, ubishi, mkabala na ufifizaji na uzidishaji. Urejelezi ulitumiwa na makundi ya kijamii kila mojawapo likirejelea kundi pinzani kupitia mkabala wa kimatendo.

Ingawa serikali ya Kenya na za kimataifa zilirejelea kundi la Al-Shabaab kama kundi la kigaidi kutokana na matendo yake ya mauaji wa raia na uharibifu wa mazingira, Al-Shabaab kwa upande wake liliona mataifa ya Kenya, Somalia, Uganda na Uhabeshi pamoja na vikosi vya shirikisho la muungano wa nchi za Kiafrika, AMISON na kimataifa kama magaidi kutokana na matendo yao. Kila kundi lilirejelea lingine kwa kuliona kama linabaguliwa kutokana na itikadi.

Unominishaji ulibainika kwa kila kundi kutokana na mtazamo wa msemaji. Kwa kutumia viwakilishi kama vile: huyu, yule, hawa, ubishi ulijitokeza kwa kutumia maneno ya kushawishi, kuomba, kudai kupitia matumizi ya chuku, upotoshi, na propaganda pamoja na kitezi neno katika kuapiza, kudai na kutangaza. Unominishajia ulitegemea mnenaji alivyomsawiri mlengwa wake. Maneno kama mdhalimu, mkiukaji wa haki, mzalendo, muuaji, mtetezi wa haki, mwenye utu na mharibifu yalitegemea mtazamo wa msemaji kumrejelea mpokezaji. Matumizi ya maneno ya mrejelewa yalijikita katika mkabala wa kiitikadi. Mkakati wa mkabala ulihusu mtazamo wa makundi haya ya kijamii. Kila mojawapo wa kundi lilitazama mwenzake kulingana na maoni na msimamo wake. Hali hii ilileta matumizi ya maneno ya ubaguaji na utengano kama vile matumizi ya "sisi "dhidi ya 'wale', maneno ya uzalendo, umoja, ushirikiano, upendo, ukatili, ukiukaji wa haki, chuki na wivu yalitumiwa kwa kutegemea mkabala wa msemaji katika muktadha. Mkabala wa kimtazamo ulizua ubishi katika muktadha wa mawasiliano kwa kutegemea msemaji alikuwa ni nani na alikuwa akimwambia nani. Mtazamo wa kimkabala ulifanya kundi moja kujiona bora kuliko lingine kupitia itikadi za kimaoni kiimani na kidini. Mkakati wa ubishi ulitokana na jinsi makundi ya kijamii yalijipata katika ugomvi kutokana na misimamo ya madai walioshikilia.

Lugha ilitumika kama mkakati wa diskosi uliozua ubishi kati ya makundi kutokana na misimamo tofauti. Matumizi ya lugha yalitegemea maneno ya msemaji dhidi ya mlengwa. Kila kundi likiongozwa na mkabala na itikadi lilitumia mbinu mbalimbali za kujitetea, kushawishi, kulaumu, kuapiza, kukuza, kukashifu, kukubali na kukataa.

Baadhi ya mbinu zilizotumiwa ambazo zilijikita katika muktadha wa ubishi zilihusu matumizi ya propaganda, chuku, upotoshi topoi na vitenzi neni. Vitenzi neni vilitumiwa kuongezea nguvu na uzito katika mawasiliano kama vile kutoa kauli, kutisha, kuamrisha, kutoa onyo, kukaripia na kulazimisha jambo. Magazeti yalionyesha jinsi makundi yalitumia mbinu hizi katika mgogoro wa ugaidi kutokana na mkabala wa msemaji.

Mikakati ya kufifiza kundi moja na kulidhalilisha liwe dhaifu kuliko lingine ilitumiwa na kurekodiwa katika magazeti. Mikakati ya kuzidisha ilitumiwa kupitia matumizi ya chuku na upotoshi kule ambako kila moja wapo ya kundi lilijipa sifa na kujigamba kuwa lilikuwa lenye uwezo mkubwa kuhusiana na ugaidi.

Nchi ya Kenya na Marekani zilijidai kuwa zilikuwa na nguvu ya kifedha, kijeshi na vifaa vya kivita ilihali kundi la Al-Shabaab kwa upande wake lilijidai kuwa liliweza kushambulia maeneo makubwa na muhimu kwa serikali ya Kenya na kusababisha hasara kubwa ya mauaji na uharibifu wa mali na rasilimali. Kila mojawapo wa makundi lilijitangaza kupitia vyombo vya habari kwa kujikuza huku likidhalilisha kundi pinzani kuwa halikuwa na mkakati wa hali ya juu kuliko lingine kuhusiana na ugaidi.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.7.1.2301

## HITIMISHO NA MAPENDEKEZO

### Hitimisho

Kupitia msingi wa mkakati wa diskosi ya DHA (Wodak, 1909) kuhusu matumizi ya lugha, mihimili ya uarifu au unominishaji, utabiri, ubishi, urejelezi wa kibaguzi, uzidishaji na ufifizaji ilitumiwa kuhakiki na kueleza jinsi lugha ilivyotumiwa na wanajamii. Mkakati wa uarifu ulionyesha kuwa wanajamii huwaita wenzao majina yanayowahusisha na ishara na matendo yao.

Kundi moja lililiita lingine gaidi ingawa matendo waliotekeleza yalitumia itikadi zilezile zilizoashiriwa kwa "magaidi". Mkakati wa urejelezi ulibainika kupitia maneno ya vitisho vya Al-Shabaab dhidi ya serikali ya Kenya kuwa ikiwa Kenya ingekataa kuyatoa majeshi yake nchini Somalia, mashambulizi mengine makubwa zaidi yangelitokea. Al-Shabaab ilitoa kauli zilizoonyesha ishara ya kuwa ilikuwa tayari kwa vita na mashambulizi mengine dhidi ya Wakenya.

### Mapendekezo

Kuna haja ya kuendeleza utafiti huu wa kidiskosi ya ugaidi kupitia makundi mengine ya kigaidi barani Afrika yaliyo na mahusiano sawa na sifa kama zile za Al-Shabaab. Baadhi ya makundi haya ya kigaidi ni kama vile: Boko Haram katika maeneo ya Nijeria, Nijer, Chad na Cameroon, Ansar Al-Sharia katika maeneo ya Tunisia na Libya na Jam'at Nusrat Al-Islam wal'Muslimin katika maeneo ya Mali na Bukina Farso. Utafiti zaidi waweza kufanywa kwa kutumia mbinu nyingine ya utafiti kama vile ya mahojiano ya moja kwa moja. Kwa kuwa waandishi wa magazeti ni zao la wanajamii, kuna uwezekano wa kupendelea kutokana na mkabala wa mwandishi kiitikadi na kimtazamo.

## MAREJELEO


Abdi, F.W. (2023). *Kenya: Five Civilians Killed, Some Beheaded In Al-Shabaab Attack In East*. https://www.africanews.com/2023/06/26/kenya-five-civilians-killed-some-beheaded-in-shebab-attack-in-east//

Abdisaid, M. A. (2008). *The Al-Shabaab Al-Mujahidiin: A Profile of the First Somali Terrorist Organization,* Institutfür Strategie Politik Sicherheits und Wirtschaftsberatung (ISPSW).

Aḥmad, H., & Azzam, S. (1976). *Islam: Its Meaning and Message*. Islamic Council of Europe.

Anwar, T. B. (2009). *The Language of Terrorism: Al-Jazeera and the Framing of Terrorism Discourse.* Georgetown University.

Blommaert, J. (2005). *Discourse. A Critical Introduction*. Cambridge University Press.

Bourdieu, P. (1991). *Language and Symbolic Power*. Harvard University Press.

Chomsky, N. (2004). *Language and Politics*. Library of Congress.

Cole, D. (2003). *Enemy Aliens: Double Standards and Constitutional Freedoms in the War on Terrorism.* New Press.

Ditrych, O. (2014). *Training the Discourses of Terrorism: Identity, Geneology and State*. Palgrave, Macmillan.

Eemeren, F.H. (2014). *Handbook of Argumentation Theory*. Springer.

English, R. (2009). *Terrorism: How to Respond.* Oxford University Press, Inc.

Exposito, J. L. (2002). *Unholy War: Terror in The Name of God*. Oxford University Press.

Fairclough, N. (1989). *Language and Power*. Longman Group (UK) Ltd.

Fairclough, N. (2003). *Analysing Discourse: Textual Analysis for Social Research*. Routledge.

Fischer, A. (2004). *The Logic of Real Arguments*. Cambridge University Press.

Friedlander, R. A. (1989). The origins of international terrorism: A Micro Legal-

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.7.1.2301


Historical Perspective. *Israel Yearbook on Human Rights*, *6*(1976), 49–61. https://doi.org/10.1163/9789004422872_003

Goodin, R. E. (2006). *What's wrong with Terrorism?* Cambridge: Polity Press

Halliday, F. (1996). *Islam and the Myth of Confrontation*. I.B Tauris.

Hansen, S.J. (2013). *Al-Shabaab in Somalia: The History and Ideology of a Militant Islamic Group*. Oxford University Press.

Hiro, D. (2002). *War without End: The Rise of Islamic Terrorism and Global Response*. New York: Routledge.

Hoffman, B. (2006). *Inside Terrorism* (REV-Revised, 2). Columbia University Press. http://www.jstor.org/stable/10.7312/hoff12698 https://www.researchgate.net/publication/241176170

Huhtamo, E. (2011). *Dismantling the Fairy Engine: Medieval Achaeology as Topois Study*. California University Press.

Jackson, R. (2014). *Constructing Enemies: 'Islamic Terrorism'in Political and Academic Discourse-Government and Opposition*. Routledge.

Jackson, R. (2016). *Routledge Handbook of Critical Terrorism*. Routledge.

Johnson, H. R. (2000). *Manifest Rationality: A Pragmatic Theory of Argument.* Lawrence Erlbaum.

Jowett, G, & O'Donnell, V. (2006). *Propaganda and Persuasion*. ISBN 1412908981, 9781412908986. SAGE.

Kress, G. & Hodge, B. (1979). *Language as Ideology*. Routledge.

Kress, G. (1985) *Linguistic Processes in Sociocultural Practice*. Oxford University Press.

Lacquer, W. (2001). *The New Terrorism.* Phoenix Press.

Meyer, M. (2001*). Between Theory, Method, and Politics: Positioning of the Approaches of CDA.* In R. Wodak, & M. Meyer (Eds.), Methods of Critical Discourse Analysis (pp. 14-32). Sage.

Michael H. F. (2005*). Introduction to Classical Legal Rhetoric*. Ashgate

Miller, D. (2004). *Tell Me Lies: Propaganda and Media Distortion in the Attack on Iraq*. Pluto. http://www.plutobooks.com/whatsnew.shtml

Mouna, B. (2021). Critical Discourse Analysis on the Representation of Muslims in Britain in the Daily Mail Newspaper: *International Journal of Language and Literary Studies, 3*(3)2021. http://doi.org/10.36892/ijlls.v3i3.624

Oando, S., & Achieng. S. (2021). An Indigenous African Framework for Counterterrorism: Decolonising Kenya's Approach to Countering "Al-Shabaab-ism", *Critical Studies on Terrorism*, *14*(3), 354-377, https://doi.org/10.1080/17539153.2021.1958182

Odhiambo, S. (2014). *Uchanganuzi wa Matini za Kigaidi Katika Gazeti la Taifa Leo. Muswada wa Uzamifu* (Phd): Maseno University.

Reah, D. (2002). *The Language of Newspapers*. Routledge.

Reisigl, M. & Wodak, R. (2001). *Discourse and Discrimination: Rhetorics of Racism and Antisemitism*. Routledge.

Rohan, G. (2005). *Current Trends in Islamist Ideology: Al-Qaeda"s Ideology, Center on Islam Democracy and the Future of the Muslim World*. Hudson Institute.

Ross, J. I. (2006). *Political Terrorism: An Interdisciplinary Approach*. Peter Lang.


 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.7.1.2301


Rutherford, P. (2000). *Endless Propaganda.* University of Toronto.

Ryan, G. & Bernard. H. R. (2003). Techniques to Identify Themes. *Field Methods*, *15*(1): 85-109.

Ryszard, P.K. (2011). *An Introduction to Topois Theory*. University of Warsaw.

Sam, L. (2012). *Words like Pistols: Rhetoric From Aristotle to Obama.* Basic Books.

Schmind, A. (1988). *Political Terrorism: A Research Guide to Concepts, Theories, Databases and Literature*. Transaction Books.

Schmind, A. (2005). *Terrorism as Psychological Warfare. Democracy and Security: Armsterdam.* Transaction Books.

Scollon, R. (1998). *Mediated Discourse as Social Interaction: A Study of News.Discourse.* Longman.

Searle, J. R. (2005). *Expression and Meaning: Studies in the Theory of Speech Acts*. Cambridge University Press.

Sharples, R.W. (2001). *Who's Aristotle? Who's Aristotlelianism?* Ashgate.

Stanley. C. B. (2002). *The Idea of Propaganda: A Reconstruction*. Praeger

Toomey, M., & Singleton, B. E. (2014b). The post-9/11 "terrorism" discourse and its impact on Nonstate Actors: A Comparative Study of the LTTE and Hamas. *Asian Politics & Policy*, *6*(2), 183–198. https://doi.org/10.1111/aspp.12110

Toulmin, S. (1950). *The Uses of Argument*. Cambridge University Press.

Unvar, S., & Rahim, A. (2013). A Critical Discourse Analysis of Discursive Structures in a Political Text, Turkey: *International Journal of Science and Advanced Technology.3* (3), 12-19

Van Dijk, T. A. (1984). *Prejudice in Discourse: An Analysis of Ethnic Prejudice on Cognition and Conversation.* J. Benjamins.

Van Dijk, T. A. (2000a). *Ideology and Discourse: A Multidisciplinary Introduction. Barcelona.* Pompeu Fabra University.

Van Dijk, T. A. (2000b). *On the Analysis of Parliamentary Debates on Immigration. In M. Reisigl, & R. Wodak (Eds.), the Semiotics of Racism: Approaches to Critical Discourse Analysis*.Vienna. Passagen Verlag.

Van Dijk, T., A. (2001). *Multidisciplinary Critical Discourse Analysis: A Plea for Diversity. In R.Wodak & M. Meyer (eds.), Methods of Critical Discourse Analysis.* Sage.

Van Dijk, T.A. (1984). *Prejudice in Discourse*. John Benjamins.

Van Dijk, T.A. (1991). *Racism and the Press.* Routledge.

Van Dijk, T.A. (1991). *The Interdisciplinary Study of News as Discourse.* Routledge.

Van Dijk, T.A. (2006). *Discourse and Manipulation: Discourse and Society.* Routledge.

Van Dijk, T.A. (2008). *Discourse and Context: A Sociocognitive Approach.* Cambridge University Press.

Van Dijk, T.A. (2008). *Discourse and Power: Contribution to Critical Discourse Studies.* Palgrave Macmillan.

Van Eemeren, F. H, Grootendorst, R., & Snoeck Henkemans, A. (2002). *Argumentation: Analysis, Evaluation, and Presentation*. Sage.

Van Eemeren, F.H. & Grootendorst, R. (1992). *Argumentation, Communication and Fallacies: A Pragma-Dialectical Perspective*. Erbaum.


This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.7.1.2301

Van Eemeren, F.H. (2009). *Examining Argumentation in Context: Fifteen Studies on Strategic Maneuvering*.John Benjamins.

Vito D'Orazio, Salehyan, I. (2018). *Who is a Terrorist? Ethnicity, Group Affiliation, and Understandings of Political Violence*. International Interactions.

Walton, D. N (2013). *Methods of Argumentation*.Cambridge University Press.

Walton, D.N (1995). *A Pragmatic Theory of Fallacies, Tuscaloosa*. University of Alabama Press.

Walton, D.N (1998). *Ad hominem Arguments, Tuscaloosa*. University of Alabama Press.

Walzer, M. (2004), *Arguing About War, New Haven and London*.Yale University Press

Wodak, R. (2009c). *Politics as Usual'- The Construction and Presentation of Politics in Action*. Palgrave Macmillan.

Wodak, R. & Krzyz'anowski, M. (2008) *Qualitative Discourse Analysis in the Social Sciences. Basingstoke*.Palgrave.

Wodak, R. & Meyer, M. (2001). *Methods of Critical Discourse Analysis.* Sage Publishers.

Wodak, R. & Meyer, M. (2009). *Methods of Critical Discourse Analysis.* Sage Publishers.

Wodak, R. (1995). *Critical Linguistics and Critical Discourse Analysis', in J. Vershueren, J-O Ostman and J. Blommaet (eds). Handbook of Pragmatics Manual*, (240-210). John Benjamins.

Wodak, R. (2001). *The Discourse-Historical Approach. In R. Wodak, & M. Meyer (Eds.) Methods of Critical Discourse Analysis (pp. 63–94)*. Sage.

Wodak, R. (2008). *'Us" and "Them" Inclusion and Exclusion-Discrimination via Discourse.* Liverpool University Press.

Wodak, R. (2009). *Critical Discourse Analysis: History, Agenda, Theory, and Methodology*. Sage Publishers.

Wodak, R. (2015). *The Politics of Fear: What Right-Wing Populist Discourses Mean*. Sage Publishers.

Wodak, R., de Cillia, R., Reisgl, M. & Liebhart, K. (2009b). *The Discursive Construction of National Identity*. Edinburgh University Press.

Woods, J. (2013). *Errors of Reasoning: Naturalizing the Logic of Inference.* College Publications.

Yazdan, S. (2016). *Positive and Negative Presentation: The Manipulation of Ideology in Translation of Iranian Political News Titles*. Kharazimi Higher Institute of Science and Technology.